M11/1/A1SWA/SP1/SWA/TZ0/XX

22110299

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SWAHILI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Wednesday 11 May 2011 (morning)
Mercredi 11 mai 2011 (matin)
Miércoles 11 de mayo de 2011 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only. It is not compulsory for you to respond directly to the guiding questions provided. However, you may use them if you wish.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Rédigez un commentaire sur un seul des passages. Le commentaire ne doit pas nécessairement répondre aux questions d'orientation fournies. Vous pouvez toutefois les utiliser si vous le désirez.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento. No es obligatorio responder directamente a las preguntas que se ofrecen a modo de guía. Sin embargo, puede usarlas si lo desea.


© International Baccalaureate Organization 2011

*Toa maoni yako juu ya* ***moja*** *ya tungo zifwatazo.*

**1.**

“Hebu huko!” Yule sista alifoka akimtumbulia utingo wa ile daladala jicho kali,” eh, ndio nini utunukie sawa na buti la mgambo?

Kauli ya sista iliimbua vicheko vya wanafunzi waliokaa kiti cha nyuma cha daladala hiyo. Walianza kunong’onezana.

“Kweli anuka kama mkojo! Kwani maji yauma?”

“Aisee, kwani kukoga tu kunahitaji pasi?”

“Jamani, hawa jamaa itabidi waogeshwe kwa nguvu kama wanavyofanywa huku Nairobi!”

Kwa ujumla, mle daladalani mlinuka vundo la ajabu: Mchanganyiko wa jasho la mwili, kwapa, mafusho na marashi ya kila sampuli. Harufu ya kupandisha roho kooni ilihanikiza kote. Abiria walilalamikia hali hiyo.

“Fungueni madirisha basi jamani!” Mama mmoja aliyempakata mtoto mchanga alisihi, “naona mwanangu yuatweta kwa joto hili!”

Kila abiria aliyekaa kiti cha dirishani, akawa anang’ang’ania kufungua vioo vya madirisha. Machache yalikubali; mengi yakadinda.

“Nd’o nini hii? Utunukie, na gari lako mbovu – madirisha hayafunguki! Kwani daladala hii ni ya wafungwa?” Sista akazidi kumpakia yule utingo aliyejining’inia mlangoni, tako nje. Vicheko zaidi.

“Sista, naomba tuheshimiane!” Utingo akajitia kumaka japo ilikuwa wazi, hakujali wala kubali.

“Nyoo, mtusheheneze sawa na mifuko ya vitunguu!” Sista alisema akijitengeneza mtandio wake kichwani.

“Sista hivi kweli, kama lilikuwa gari la mbinguni, ungelitaahari kuliabiri!” Utingo sasa, akaanza vituko vyake-wakitajika sana kwa vita vya maneno.”

“Hivi unadhani mbinguni mtakwenda nyie? Watu hata staha kwa watumishi wa Mungu, kina mama na watoto, hamna?” Maneno ya sista yakashika njia nyingine. Kitu kama mahubiri vile. Lakini ifae nini?

“Kwani sisi hapa twafanya kazi ipi? Si tuwapeleke watu wa Mungu makwao wakajipumzishe machovu ya kutwa?” Falsafa ya utingo nayo, ikadhihiri.

“Kazi sista, ni kazi. Baadhi yetu tunafanya kazi za sulubu zaidi ya kuzembea ati mtu aabudu. Ibada tu bila kazi zitupeleke wapi?” Mwanamume mmoja aliyevalia surupwenye yenye mavumbi ya saruji alijitia katika mjadala.

“Kweli kabisa. Kazi ni sawa na ibada!” Zilisikika kwa abiria wengi.

“Lakini mtu akae kutwa nzima akisoma rosari, jioni aaingie garini awalaumu waliotokwa na jasho la kutafutia huo ugali na dagaa!” Sasa utingo akapata moyo; sista alihitaji afundishwe kuishi kwa uhalisi.

“Kazi si uchafu utingo! Mtu ni usafi-hata huku huwaoni wakioga kwa udongo?” Sista akajitetea kwa kuelekeza lawamana shutuma kwa wengine.

“Sanawari! Sanawari wapo?” Utingo alisema, gari lilipofika barabara ya kuteremshia *Arusha International Conference Centre* sauti kadhaa ziliitika. Dereva alisimamisha gari.

“Naomba unisaidiye huyu mtoto nishuke,” mama aliyeketi na yule sista alisikika akisema. Akamkabidhi sista kibegi kidogo; sista akakiangika begani, kisha akampokea yule mwana. Utingo alikuwa akiwatolea abiria mizigo unyende uliposikika.

“Simu yangu imeibwa!” Yule mama aliyesaidiwa na sista alihanikiza.

“Ashindwe! Shetani ashindwe!” Sista alisema, huku akifanya ishara ya msalaba kwa mkono.

“Toba! Hivi tutanusurika lini na hawa vibaka? Pole sana dada, stesheni hii yahitaji ulinzi zaidi,” mzee mmoja alimfariji yule mama mtoto.

Utingo akaingia garini, akaanza kupekua ndani ya gari. Hakuipata.

“Jamani eh, pana mtu aliyeona simu ya mwenzetu hapa?” Kimya.

“Bwana we, haya ni mambo ya kawaida? Dereva endesha, twachelewa!” Mtu mmoja huku nyuma alisikika akisema.

“Twende! Kwani simu ni mtoto? Si ana mwanawe?” Mwingine alidakia. Vicheko.

PI Iribemwangi, *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2007)

- Malumbano yanayojitokeza kwenye kifungu hiki yanadhihirisha sifa zipi za wahusika?
- Ni mbinu zipi za lugha zinazojitoke kwenye kifungu hiki?
- Maudhui yanayojitokeza yanaathiriwa kivipi na mazingira kwenye kifungu hiki?
- Onyesha umuhimu wa lugha katika kupitisha ujumbe wa mwandishi.

**2.**

**Ukizini Umetenda Dhambi Kubwa**

Kweli wako utafiti, ndungu yangu Alamini,
Utokapo shoti, ulekeapo kazini,
Unapigiwa magoti, watendewa abautani,
Usicheze na wakati, dhambi kubwa ukizini.

Unapopata wakati, kumchota wa ndiyani,
Akuliwazapo siti, kukuenzi faraghani,
Wakiwasha kibiriti, wajiunguza motoni,
Usicheze na wakati, dhambi kubwa ukizini.

Uwaonapo banati, wang'arao mitaani,
Maabaya huyaseti, yakawakaza mwilini,
Wapasua katikati, vya kati vikabaini,
Usicheze na wakati, dhambi kubwa ukizini.

Nale wa minisketi, wazururao ndiani,
Huzikazisha taiti, p'liti za viunoni,
Na kufupisha tishati, wawazi vitovuni,
Usicheze na wakati, dhambi kubwa ukizini.

Usijifanye smati, kijimbi cha m'taani,
Apitae humuati, kwa ashiki ya shetani,
Waja juta na laiti, ujingize majozini,
Usicheze na wakati, dhambi kubwa ukizini.

Ukimwi umezatiti, hauna dawa yakini,
Ulengapo guruneti, ni mlipuko wa zani,
Dunia hutaketi, waishia kaburini,
Usicheze na wakati, dhambi kubwa ukizini.

Ogopa uasharati, mkumbuke Rahamani,
Kaowe na ailati, mwenye heshima na dini,
Uzipate hasanati, akhera na dunia,
Usicheze na wakati, dhambi kubwa ukizini.

Watamati kalimati, nimefika kikomoni,
Umenishia wakati, nakimbilia kazini,
Mkumbuke jabaruti, usijute baadeni,
Usicheze na wakati, dhambi kubwa ukizini.

Swaqleh Abeid, *Taifa Leo* (2010)

- Mwandishi wa shairi hili anamsimamo upi kuhusu mavazi yanayo valiwa na wasichana?
- Mwandishi ametumia mbinu ipi ili kufanikisha upitishaji wa ujumbe wake?
- Onyesha vile mtindo wa mwandishi unavyomsaidia katika kuendeleza mawazo yake.
- Mwandishi ana maoni gani kuhusu umuhimu wa wakati katika shairi hili?